

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S. L.P 30261

Kibaha.

Simu: (023) 2402658

Nukushi: (023) 2402657

Baruapepe: [rbcpwani@pccb.go.tz](mailto:rbcpwani@pccb.go.tz)

Wavuti : [www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

TAARIFA KWA WANANCHI KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

PWANI - FEBRUARI 5, 2021

TAKUKURU MKOA WA PWANI YAMNASA MTUMISHI WA DAWASA KIBAHA  
AKIPOKEA HONGO YA SH. 220, 000/=

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Pwani imemkamata Bw. Gidman Bishingwa Athanas mtumishi wa Dawasa Kibaha kwa kuomba hongo ya kiasi cha **Shilingi Laki Mbili na Ishirini (Sh. 220,000/=)** kutoka kwa Mlalamikaji (jina linahifadhiwa) mkazi wa Picha ya Ndege eneo la Umwalani Wilaya ya Kibaha Mji ili asiwasilishe taarifa ya deni la mlalamikaji ofisini alilodai kuwa ni Sh. 500,000/= (laki tano).

Ofisi ya TAKUKURU (M) Kibaha ilipokea malalamiko hayo mnamo tarehe 03, Februari, 2021 ambapo uchunguzi ulijiridhisha kwamba, ni kweli Bw. Gidman Bishingwa Athanas alitaka fedha hizo za hongo, hivyo mtego uliandaliwa mnamo tarehe 04/02/2021 na kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa huyo akipokea fedha kiasi cha Sh. 220,000/= nyumbani kwa Mlalamikaji (jina tunalihifadhi) eneo la Picha ya Ndege, Umwalani Kibaha Mji. Kosa hili ni kinyume na Kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana a Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007.

Uchunguzi wa tuhuma hii bado haujakamilika na baada ya kukamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zake.

**WITO**

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, Bi SUZANA RAYMOND anawaasa watumishi wote katika mkoa wa Pwani wafuate sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali pamoja na taasisi zao ili kuepusha malalamiko kwa wananchi. Tunaomba pia wananchi waendeleo kuwafichua watu wote wanaoomba rushwa kwa kutoa taarifa TAKUKURU ili hatua ziweze kuchukuliwa kwa wale watumishi wanao kahidi kufuata sheria na kanuni za kazi.

***KATAA RUSHWA JENGA NCHI YAKO***

Imetolewa na:

*SUZANA RAYMOND,*

*MKUU WA TAKUKURU MKOA WA PWANI*

0738150176